# HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 19/10/2021

### MAHUDHURIO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg.Marclaud J.Mero | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Paul M.Mafuru | Katibu |
| 3. | Ndg. Bi. Mwema D. Salum | Mjumbe |
| 4. | Ndg. Kalokola P.Kasimbazi | Mjumbe |
| 5. | Dr. Gabriel Mashauri | Mjumbe |
| 6. | Bi. Zainabu K. Ally | Mwanasheria |
| 7. | Ndg. Deogratias I.Bugenyi | Sekretarieti |

### WASIOKUWEPO

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Lucas H.Daud | Mjumbe | Kwa taarifa |

### AGENDA

1. Kufungua Kikao.
2. Kupitisha agenda za Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha mhitasari wa kikao
4. Yatokanayo na Kikao kilichopita cha tarehe 23/09/2021
5. Kujadili na kupitisha mapendekezo ya utaratibu wa force akaunti kutumika katika miradi inayogharimiwa na fedha za UVIKO-19
6. Kuidhinisha Wazabuni wa Vifaa mbalimbali
7. Kufunga Kikao.

**Muhtasari Na.01/10/CTB/2021-2022: Kufungua Kikao**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 02:38 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao na baada ya hapo katibu alimkaribisha mwanafunzi wa Mazoezi kwa vitendo katika fani ya ununuzi kujitambulisha ili wajumbe wamfahamu.

**Muhtasari Na.02/10/CTB/2021-2022: Kupitisha agenda za kikao.**

Jumla ya agenda saba (9) zilisomwa na katibu kasha zilithibitishwa na Wajumbe wote kuwa agenda halali za kikao.

**Muhtasari Na.03/10/CTB/2021-2022: Kusoma na Kuthibitisha Mhitasari wa Kikao kilichopita cha tarehe 23/09/2021.**

Katibu alisoma Muhtasari wa kikao mbele ya wajumbe na kuthibitishwa kuwa kumbukumbu halali ya kikao cha Bodi ya Zabuni ya Halmashauri.

**Muhtasari Na.04/10/CTB/2021-2022: Yatonayo na Kikao cha tarehe 23/09/2021.**

**Azimio :** Wajumbe waliazimia kutangaza Zabuni za Usambazji na Uuzaji wa Vifaa vya Viwandani na ofisini kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri kwa kutumia Mfumo wa Kimanunuzi wa Kietroniki (TANePS)

**Utekelezaji:** Zabuni Namba LGA/032/2021-2022/HQ/G/LOT.1 kwa ajili ya usambazaji na uuzaji wa vifa vya ujenzi mchanganyiko (Industrial building materials) na Zabuni namba LGA/032/2021-2022/HQ/G/LOT.2 ya usambazaji na uuzaji wa vifaa vya umeme kwa ajili kufunga mfumo wa umeme zilitangazwa kwenye mfumo.

**Muhtasari Na.05/10/CTB/2021-2022: Kujadili na kupitisha mapendekezo ya utaratibu wa force akaunti kutumika katika miradi inayogharimiwa na fedha za UVIKO-19**

Katibu wa Bodi aliwasilisha mapendekezo ya kutumia utaratibu wa force akaunti katika miradi inayogharimiwa na fedha za UVIKO-19 kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa ili kumaliza miradi kwa wakati. Fedha hizo zimetumwa kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Tsh 1,820,000,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba 91 vya madarasa kwa shule za Sekondari 20.

ii. Tsh 1,360,000,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba 68 vya madarasa kwa shule shikizi za Msingi 17.

iii. Tsh 90,000,000.00 kwa ajili Ujenzi wa nyumba ya Watumishi wa Afya 3:1

iv. Tsh 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Bweni (Elimu Msingi)

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:**

**Mjadala**

**Wajumbe walihoji juu ya ngazi ambapo utekelezaji wa miradi utafanyikia**

Katibu wa Bodi alitoa maelezo kwamba fedha zimeingizwa kwenye akaunti ya kila taasisi hivyo watafanya wenyewe kwa kusimamiwa na Wataalam wa Halmashauri.

**Maamuzi:**

Baada ya kupitia na kujadili mapendekezo ya utekelezaji wa miradi inayogharimiwa na fedha za UVIKO-19, Wajumbe wa Bodi waliazimia ufanyike kwa kutumia utaratibu wa force akaunti na kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa pamoja na sheria na kanuni za ununuzi wa umma.

**Muhtasari Na.06/10/CTB/2021-2022: Kuidhinisha Manunuzi Mbalimbali**

**Maombi ya Manunuzi Yaliyopokelewa**

Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Ugavi kimepokea maombi yaliyoidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa ajili ya kufanya manunuzi ya vifaa mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Ununuzi wa Tairi za Gari kupitia Requisition for Purcahse yenye Namba 2004 ya tarehe 9/10/2021 ya kutoka Idara ya fedha ya Gari SM 6934.

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:** Ununuzi wa tairi ufanyike kwa njia ya ushindani kupitia mfumo wa TANePS

(ii) Ununuzi wa Huduma ya Uchapishaji wa Mitihani kupitia Requisition Na.005931 kutoka Idara ya Elimu Msingi ya tarehe 02/10/2021

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:** Ununuzi wa huduma ya uchapishaji wa mitihani ufanyike kwa njia ya ushindani kupitia vidadisi bei kwa watoa huduma wanaopatikana katika eneo la Wilaya ya Biharamulo.

(iii)Ununuzi wa Shajala za Idara ya Utawala kupitia Requisition Na.1761 ya tarehe 23/09/2021.

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:** Manunuzi yashindanishwe kupitia katika mfumo wa Kimanunuzi wa Kiekitroniki (TANePS).

**Manunuzi yaliyofanyiwa tathmini kupitia mfumo wa TANePS**

✓ Ununuzi wa Antivirus Idara ya Ujenzi, Kilimo pamoja na Ununuzi wa Shajala Idara ya Utawala. Manunuzi haya baada ya kutangazwa kupitia mfumo wa TANePS yaliombwa na Watoa huduma Wawili tu ambao ni Quadratic Supplies wa S.L.P 240 Karagwe kwa jumla ya Tsh 5,720,000.00 na Ruchy Computer Company wa S.L.P 1879 Bukoba kwa bei ya Tsh 7,846,000.00. Wazabuni wote wawili walionekana wamekidhi vigezo vyote vilivyowekwa kwenye nyaraka ya zabuni baada ya kufanya tathmini kupitia mfumo wa TANePS ambapo Mzabuni Quadratic Supplies wa S.L.P 240 Karagwe alionekana ametoa kotesheni ya chini kabisa ukilinganisha na Ruchy Computer Company wa S.L.P 1879 Bukoba.

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:** Bodi ya zabuni inakubaliana na mapendekezo yaliyo kwenye taarifa ya tathmini ya kumtunuku mkataba wa Usambazaji wa Vifaa mzabuni Quadratic Supplies wa S.L.P 240 Karagwe kwa jumla ya gharama ya Tsh 5,720,000.00

✓ Ununuzi wa wa Shajala Idara ya Afya. Manunuzi haya yalitangazwa kupitia mfumo wa TANePSA na kuombwa na Watoa huduma Wawili tu ambao ni Kichemu General Supply wa S.L.P 326 Bukoba kwa jumla ya Tsh 52,809,500.00 na Monavale Geneal Supply wa S.L.P 1625 Bukoba kwa bei ya Tsh 2,765,000.00. Wazabuni wote wawili walionekana wamekidhi vigezo vyote

vilivyowekwa kwenye nyaraka ya zabuni baada ya kufanya tathmini kupitia mfumo wa TANePS ambapo Mzabuni Monavale Geneal Supply wa S.L.P 1625 Bukoba alionekana ametoa kotesheni ya chini kabisa ukilinganisha na za mwingine.

**Mjadala na Maamuzi ya Bodi ya Zabuni:** Bodi ya zabuni inakubaliana na mapendekezo yaliyo kwenye taarifa ya tathmini ya kumtunuku mkataba wa Usambazaji wa Vifaa mzabuni Monavale Geneal Supply wa S.L.P 1625 kwa gharama ya Tsh 2,765,000.00

**Muhtasari Na.07/10/CTB/2021-2022: Kufunga Kikao**
Mwenyekiti alifunga kikao saa 10:05 Jioni na aliwashukuru na kupongeza wajumbe kwa mjadala waliofanya kwa makini na mwisho aliwatakiwa wajumbe utekelezaji mwema wa majukumu ya kifamilia na Kiserikali.

**Umethibitishwa**

..................................................
**Katibu**

..................................................
**Mwenyekiti**

21/01/2022
..................................................
**Tarehe**